BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

<u>BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI</u>

<u>MKUTANO WA KUMI NA TANO</u>

<u>Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 19 Juni, 2024</u>
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. <u>MASWALI:</u>

### <u>Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:</u>

250. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Je, kuna tathmini yoyote iliyofanywa na kuonesha wastani wa viwango vya mvua na kiwango cha ongezeko la joto kwa mwaka 2023/2024

### <u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa. Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

59. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Hivi karibuni kumeripotiwa matukio kadhaa ya wananchi kuzama baharini katika maeneo ya bahari ya visiwa vya Unguja na Pemba. Matukio hayo yameonesha kuwa kuna haja ya kuwa na vyombo vya utayari vya uokozi katika bahari zetu hasa kwenye maeneo ya kuvukia kama vile Kisiwa Panza, Tumbatu, Uzi na mengineyo.

(a) Je, Serikali inao mpango wa baadae wa kuwa na vyombo maalumu vya utayari wa kukabiliana na majanga ya wananchi wanaozama baharini.

(b) Kwa kuwa nchi za wenzetu zinaweka mikakati ya utayari wa kukabiliana na majanga ya baharini, je, Serikali yetu ina mpango wowote wa kuweka mikakati hiyo kama vile kuweka wazamiaji maalumu na vyombo vya uokozi vinavyoweza kufanyakazi hata nyakati za usiku.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

132. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Sheria ya Kodi ya Majengo (Property Tax Act), Na. 14 ya 2008, inamtaka kila mmiliki wa jengo la biashara kulipa Kodi ya Jengo kwa mujibu wa Sheria hii. Pamoja na takwa hilo la kisheria, bado kumekuwa na changamoto kubwa katika kukusanya Kodi hii ya Majengo:

(a) Je, ni wafanyabiashara wangapi hulipa kodi hii tokea kutangazwa kwake na mapato kiasi gani huingia Serikalini kwa kila mwaka.

(b) Kwa kuzingatia tathmini iliyofanywa, Je, ni majengo mangapi hapa Zanzibar yanayofanya biashara na yanapaswa kulipa Kodi ya Majengo.

(c) Je, Serikali hutumia mfumo gani wa kulitambua jengo linalofanya biashara na kiwango gani cha kodi hutozwa kwa kila jengo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

78. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Msitu wa Ngezi uliopo kisiwani Pemba una maajabu mengi na vivutio vingi vya kitalii, kimoja wapo ni mti unaotoa damu unapokatwa gamba lake. Mti huo unajulikana kama mdamudamu na asili yake ni India. Hata hivyo, msitu huu hivi karibuni umekabiliwa na uharibifu wa kukatwa katwa na wananchi.

(a) Je, kuna ukweli wowote wa suala hili.

(b) Je, Wizara yako inachukuwa hatua zipi kuzuia uharibifu wa msitu huo.

**Wizara ya Afya:**

105. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la ugonjwa mbaya wa ngozi (Serodema Pigmentosum), unaowaathiri zaidi watoto, hususan wanapopigwa na jua na kuwasababishia maradhi ya kansa. Na kwa kuwa, Ripoti zinaonyesha kuwa ugonjwa huu umeathiri zaidi katika Mkoa wa Kaskazini Pemba. Na kwa kuwa, pamoja na tatizo hili kuongezeka, Serikali bado haijatoa taarifa rasmi kuhusu ugonjwa huu ambao unawasumbua wananchi kwa sasa.

(a) Je, Serikali inatambua uwepo wa ugonjwa huu, na takwimu zipo vipi kuhusu wagonjwa wa ugonjwa huu hadi sasa.

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka kuhakikisha kuwa wagonjwa walioathirika na ugonjwa huu wanapata matibabu ya haraka.

(c) Kwa kuwa wengi wa walioathirika wamepata matibabu nje ya Zanzibar, kama vile katika hospitali ya KCMC, Je, Serikali inawasaidi vipi wananchi hawa.

186. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

(a) Tathmini ikoje juu ya ongezeko la tatizo la saratani ya shingo ya kizazi.

(b) Je, kuna ukweli kwamba mwanamme ndie msafirishaji mkubwa wa kimelea cha saratani ya shingo ya kizazi.

(c) Ni ipi kinga bora ya saratani ya shingo ya kizazi itakayoweza kuwasaidia wananchi wetu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

122. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika kuboresha na kufikisha mawasiliano ya mitandao ya simu, Serikali imekuwa ikitoa vibali vya ujenzi wa minara katika maeneo mengi ya Zanzibar. Pamoja na juhudi hizi, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wataalamu kwamba minara hii hujengwa karibu sana na maakazi ya watu, jambo ambalo linahatarisha usalama wa watu kutokana na mionzi hatari inayotokana na shughuli za minara hii.

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hili na imewahi kufanya tathmini yoyote ya kitaalamu juu ya athari hizi.

(b) Je, ni mapato ya kiasi gani Serikali inaingiza kwa huduma za minara hii kutoka katika makampuni ya simu kwa mwaka.

(c) Je, ni upi mkakati endelevu wa Serikali wa kuhakikisha kuwa hakuna madhara ya kibinaadam kwa wananchi katika uwekezaji huu.

253. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tathmini iko vipi juu ya matukio ya usalama barabarani kwa mwaka uliopita hususani katika matukio ya ajali zilizosababisha vifo, watu waliokufa na watu waliojeruhiwa.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

131. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Pamoja na juhudi za Serikali katika kuunganisha umeme katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar, kumekuwa na malalamiko mengi ya waombaji wa huduma hii, ikiwa ni pamoja na ucheweleshaji mkubwa wa huduma hii kwa wananchi mpaka kupelekea mianya ya rushwa kwa watumishi wa Shirika hili la Umeme la Zanzibar (ZECO).

(a) Je, Serikali inalitambua tatizo hili la ucheleweshaji wa kufunga mita na nguzo za umeme kwa waombaji.

(b) Je, ni waombaji wangapi kwa upande wa Unguja na Pemba, ambao bado hawajapatiwa huduma hii mpaka kufikia mwezi Aprili, 01 2024.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha kuwa huduma hii inapatikana kwa haraka, ili kuwapunguzia wananchi usumbufu wa kukaa muda mrefu bila ya kuipata huduma hiyo.

<u>**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**</u>

37. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Serikali imeandaa mtaala mpya wa elimu nchini mwetu.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi katika suala zima la kutoa mafunzo juu ya mtaala huo kwa walimu wenye ulemavu.

(b) Je, Serikali ina utaratibu wowote wa kuwatambua walimu wenye ulemavu wa aina tofauti.

53. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na vyuo vyingi binafsi nchini vinavyotoa wahitimu wa afya katika ngazi na kozi mbali mbali, ikiwa ni pamoja na Glorious Academy, Zanzibar School of Health, Polytechnic College, Zanzibar College of Health na Mwenge College.

(a) Je, vyuo hivi vinatumia mitaala gani kufundishia na kwa kiasi gani Wizara yako imejiridhisha ya kuwa mtaala unaotumika ni mmoja na elimu inayotolewa mnaitambua.

(b) Kwa kuwa kuna faida kubwa ya kuwa na mtaala wetu wa afya katika vyuo vyetu vya binafsi ikiwemo usawa katika utoaji wa elimu, Je, Serikali inalifanyia kazi vipi suala hili.

(c) Je, ni kwa sababu zipi zilizoikwaza Wizara yako ikapelekea kushindwa kulifikia suala hili na kuweza kuanzisha mtaala mmoja utakaotumiwa na vyuo vyetu vya afya hapa Zanzibar.

II. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2024/2025.

Zanzibar,
19 Juni, 2024.

(Raya Issa Msellem)
<u>KATIBU WA BARAZA</u>